# MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOKETI TAREHE 25/10/2021 KATIKA OFISI YA MBUNGE WA JIMBO LA KWELA – LAELA

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:-**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Chande A. Juma | - | Afisa Ardhi na Maliasili (W) | - | Mwenyekiti |
| 2. | Bi. Mainess T. Kiluswa | - | Kaimu Afisa Manunuzi (W) | - | Katibu |
| 3. | Bi. Bahati V. Mgimwa | - | Afisa Uchaguzi (W) | - | Mjumbe |
| 4. | Bw. Joseph G. Millinga | - | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) | - | Mjumbe |
| 5. | Bw. Gibson Haonga | - | Afisa Ushirika (W) | - | Mjumbe |
| 6. | Bw. Herbert J. Mbise | - | Mwanasheria (W) | - | Mwalikwa |
| 7. | Bi. Dorah P. Sospeter | - | Afisa Manunuzi | - | Mwalikwa |

**SEKRETARIETI:-**

1. Bw. Aloyce P. Mwingo - Katibu wa Kamati

## AGENDA NA. HW/CTB/1/25/10/2021: KUFUNGUA NKIKAO

Kabla ya kufungua Kikao Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufungua Kikao.

Mwenyekiti aliwaomba Wajumbe kujadili kwa umakini na kwa utulivu, ili kuweza kutoa mapendekezo na ushauri wenye tija na manufaa kwa Halmashauri.

Baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifungua Kikao mnamo saa **06:22 mchana.**

## AGENDA NA. HW/CTB/2/25/10/2021: KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Agenda zifuatazo zilisomwa na kuthibitishwa kuwa agenda za Kikao;-

1. Kufungua Kikao.
2. Kusoma na kuthibitisha agenda.
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 21/06/2021
4. Kuidhinisha njia ya utekelezaji wa Mradi wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO – 19.
5. Kuidhinisha njia ya utekelezaji wa mradi vyoo vya WASH.
6. Kuidhinisha njia ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Afya Kipeta na Kaoze.
7. Kufunga kikao

## AGENDA NA. HW/CTB/3/25/10/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 21/06/2021

Muhtasari wa Kikao cha Bodi ya Zabuni cha tarehe 21/06/2021 ulisomwa na kusainiwa mara baada ya kuthibitishwa kuwa muhtasari sahihi.



CamScanner

**AGENDA NA. HW/CTB/4/25/10/2021: KUIDHINISHA NJIA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO – 19.**

Iliwasilishwa taarifa kuwa, mnamo tarehe 16/10/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilipokea fedha kiasi cha shilingi 2,160,000,000/= ikiwa ni fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa ni kama ifuatavyo;-

| NA. | JINA LA MRADI | FEDHA ZILIZOTOLEWA | AINA YA MRADI | MAPENDEKEZO YA MATUMIZI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa Madarasa 87 ya Shule za Sekondari kwa fedha za UVIKO 19 | 1,740,000,000 | Mpui Sekondari – madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | Uchile Sekondari madarasa 5 | 100,000,000/= |
| | | | Miangalua sekondari madarasa 5 | 100,000,000/= |
| | | | Lusaka Sekondari madarasa 4 | 80,000,000/= |
| | | | Shule ya Sekondari Kwela Madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | Shule ya Sekondari Mzindakaya madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | Shule ya sekondari Lula | 100,000,000/= |
| | | | Makuzani Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | Ilemba Madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | Kaoze Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | Kapenta sekondari 4 | 80,000,000/= |
| | | | Kikwale shule ya msingi madarasa 4 | 80,000,000/= |
| | | | Kipeta Sekondari madarasa 3 | 60,000,000/= |
| | | | Mazoka Sekondari madarasa 6 | 120,000,000/= |
| | | | Vuma Sekondari madarasa 7 | 140,000,000/= |
| | | | Milenia sekondari 6 | 120,000,000/= |
| | | | JUMLA NDOGO | 1,740,000,000/= |
| 2 | Ujenzi wa bweni 1 la Wanafunzi wenye mahitaji maalum Shule ya Msingi Mkamanye kwa fedha za UVIKO 19 | 80,000,000/= | Ujenzi wa bweni 1 | 80,000,000/= |
| JUMLA NDOGO | | | | 80,000,000/= |
| 3 | Ujenzi wa Madarasa 17 katika Shule tano Shikizi kwa fedha za UVIKO 19 | 340,000,000 | Shule ya Msingi Mwadui madarasa 5 | 100,000,000/= |
| | | | Shule ya Msingi Sofia Town madarasa 2 | 40,000,000/= |
| | | | Shule ya Msingi Kilando madarasa 2 | 40,000,000/= |
| | | | Shule ya Msingi Kikwale madarasa 5 | 100,000,000/= |
| | | | Shule ya Msingi Namonka madarasa 3 | 60,000,000/= |
| | | | JUMLA NDOGO | 340,000,000/= |
| | | | JUMLA KUU | 2,160,000,000/= |

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Wajumbe waliipitia na kupendekeza kama ifuatavyo;-



CamScanner

endekezo:-

Kutokana na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kupokea fedha za Mradi wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19 kiasi cha Shilingi 2,160,000,000/=, Bodi ya Zabuni imeridhia utekelezaji wa mradi huo ufanyike kwa njia ya "force Account" kwa utaratibu wa "Single Source" kutokana na sababu za;-

I. Jiografia ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kutokuwa rafiki na kuwa na mazingira magumu katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.
II. Mradi kuwa na ukomo wa muda uliowekwa, ambao ni vigumu kutekeleza kwa njia nyingine.
III. Fedha hizo kuletwa zikiwa na mwongozo wa kutekeleza kwa njia ya "force Account" kwa utaratibu wa "Single Source".

**AGENDA NA. HW/CTB/5/25/10/2021: KUIDHINISHA NJIA YA UTEKELEZAJI WA MRADI VYOO VYA WASH.**

Iliwasilishwa taarifa kuwa kuwa, mnamo tarehe 04/10/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imepokea fedha kiasi cha shilingi 251,900,000/= kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya WASH katika Zahanati 8. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo;-

| NA. | JINA LA MRADI | AINA YA MRADI | FEDHA ILIYOTOLEWA |
|---|---|---|---|
| 1. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Chitete | 31,487,500/= |
| 2. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Tentula | 31,487,500/= |
| 3. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Kalambazite | 31,487,500/= |
| 4. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Ilemba | 31,487,500/= |
| 5. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Msia | 31,487,500/= |
| 6. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Uzia | 31,487,500/= |
| 7. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Nkwilo | 31,487,500/= |
| 8. | UJENZI WA VYOO VYA WASH | Ujenzi wa matundu 5 ya vyoo, kichomea taka 1, shimo la kutupia kondo la nyuma, na matenki ya maji Zahanati ya Mfinga | 31,487,500/= |
| JUMLA | | | 251,900,000/= |

Kutokana na mapokezi ya fedha hizo, na kwa kuwa utekelezaji unatakiwa kuanza mara moja, Bodi ya Zabuni ilitakiwa kupendekeza njia zuri ya utekelezaji wa Mradi huo.



CS CamScanner

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Bodi ya Zabuni iliipitia kwa kina na kutoa mapendekezo kama ifuatavyo;-

**Pendekezo:-**

Bodi ya Zabuni inapendekeza Mradi wa Ujenzi wa Vyoo vya WASH katika Zahanati 8 utekelezwe kwa kutumia njia ya Mkandarasi kutokana na;-

I. Uwepo wa Miradi mingi ya UVIKO - 19 ambayo inatekelezwa kwa njia ya "Force Account".
II. Uhaba wa Wataalam wa Ujenzi wa kusimamia miradi.
III. Makisio halisi ya ujenzi wa Vyoo vya WASH kuwa makubwa kuliko fedha zilizopokelewa ambapo makisio halisi ni 48,000,000/=.
IV. Ujenzi wa vyoo vilivyopita haukukamilika kwa "Force Account" na kusababisha hoja za ukaguzi na kwa wafadhili.

**AGENDA NA. HW/CTB/6/25/10/2021: KUIDHINISHA NJIA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI WA VITUO VYA AFYA KIPETA NA KAOZE.**

Iliwasilishwa taarifa kuwa, Halmashauri imepokea fedha kutoka Serikali Kuu kiasi cha shilingi 250,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kipeta, na imetoa fedha kiasi cha shilingi 100,000,000/= kutoka katika Mapato ya Ndani kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kaoze.

Kutokana na mapokezi hayo, iliwasilishwa taarifa kwa Bodi ya Zabuni ili iweze kutoa mapendekezo ya njia ya kutumia katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, Bodi ya Zabuni ilitoa mapendekezo kama ifuatavyo;-

**Pendekezo:-**

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Vituo vya Afya Kipeta na Kaoze ufanyike kwa kutumia Wakandarasi kutokana na jiografia ya maeneo ya utekelezaji wa miradi, pamoja na uhaba wa Wataalam wa kusimamia miradi.

**AGENDA NA. HW/CTB/7/25/10/2021: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa maamuzi mazuri yatakayofanikisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati, kisha akafunga Kikao mnamo saa 08:49 mchana.

**UMETHIBITISHWA NA:**

KATIBU

Jina: Mainess Kiluswa

Sahihi. ..................................

Tarehe. 03/ 01/2022

MWENYEKITI

Jina: Chande A. Juma

Sahihi. ..................................

Tarehe. 03/ 01/2022